**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS,**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA**

*Tafadhali unapojibu taja;*

**Kumb. Na**. IMC/S.20/2/VOL II/171 19/11/2024

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa anawatangazia Watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa kuomba nafasi ya kazi iliyotajwa hapo chini, baada ya kupokea kibali chenye **Kumb Na. FA. 170/363/01A/116 cha tarehe 25 Septemba, 2024** kutoka kwa **Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Ummana Utawala Bora**.

## 1.0 MHUDUMU WA JIKONI DARAJA II- (NAFASI 4)

### 1.1 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kusafisha vyombo vya kupikia;
ii. Kusafisha vyombo vya kulia chakula;
iii. Kusafisha sehemu ya kulia chakula;
iv. Kuwatayarishia Wapishi/Waandazi vifaa vya kazi;
v. Kusafisha maeneo ya kupikia.

### 1.1.1 SIFA ZA KUAJIRIWA

Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV)

Mwenye cheti cha mafunzo ya mwaka mmoja ya Uhudumu wa Jikoni kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali

### 1.1.2 NGAZI YA MSHAHARA

Ngazi ya mshahara ni TGOS A

**MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini Serikalini;

ii. Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa

Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

iii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/ Wakili;

iv. Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.

v. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V)** yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**referees)** watatu wa kuaminika.

vi. Maombi yote yaambatane na cheti cha taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/ Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne na cheti cha kuhitimu mafunzo ya Uhudumu wa jikoni.

vii. "Testmonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne **(FORM IV AND RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**

viii. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).**

ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

x. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka **Na CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.**

xi. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

xii. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni **tarehe 02/12/2024.**



xiii. **Muhimu:** Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

**Mkurugenzi wa Halmashauri,**

**Manispaa ya Iringa,**

**S.L.P. 162,**

**IRINGA.**

v. Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; https://portal.ajira.go.tz/ (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sektretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa ‘Recruitment Portal’).

vi. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**

Tangazo hili limetolewa na;

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI**

**MANISPAA YA IRINGA.**

*Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Iringa S.L.P 162 Simu Na: 026 - 2702647, Barua Pepe:md@iringamc.go.tz, Tovuti:www.iringamc.go.tz*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI

S.L.P 42
**SINGIDA**

**Kumb. Na. IDC/B.1/8 “B”/52** **Tarehe:** 08/11/2024

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Kufuatia Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kupata kibali cha ajira mpya chenye Kumb. Na. FA. 170/366/01B/150 cha tarehe 26 Septemba, 2024 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Wilaya ya Ikungi anatangaza nafasi ya kazi na anakaribisha maombi kwa Watanzania wenye Sifa za kujaza nafasi kama ilivyoorodheshwa kwenye Tangazo hili.

### 1.0 MLEZI WA WATOTO MSAIDIZI - (NAFASI 1)

### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI:

- Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Kidato cha Sita (VI).
- Awe amefuzu mafunzo ya Astashahada/Cheti (Technician Certificate NTA level 5) katika moja ya fani zifuatazo: Elimu ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, Ustawi wa Jamii, Saikolojia kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali.

### 1.2 KAZI NA MAJUKUMU YA MLEZI WA WATOTO MSAIDIZI

i. Kushiriki kutekeleza mpango jumui wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya watoto, (ECD integrated plan);
ii. Kuandaa na kutekeleza ratiba ya shughuli za kila siku katika kituo husika;
iii. Kubainisha na kutumia mazingira salama ya kujifunzia watoto;
iv. Kutoa rufaa ya masuala ya watoto yaliyo nje ya uwezo wake;
v. Kutambua watoto wenye mahitaji maalumu na kutoa huduma stahiki;
vi. Kushiriki katika uhamasishaji wa jamii katika kutoa huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto;
vii. Kutoa ushauri kwa wazazi/walezi kuhusu malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto katika eneo lake;

viii. Kuandaa na kutoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za kila siku katika eneo husika;
ix. Kushiriki kwenye mchakato wa uendeshaji wa mashauri ya watoto katika ngazi husika (case management);
x. Kuandaa taarifa ya uanzishaji wa vituo vya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika maeneo husika; na
xi. Kufanya kazi nyingine yoyote atakayopangiwa na Mkuu wake wa kazi kulingana na elimu na ujuzi wake.

### 1.3 NGAZI YA MSHAHARA:

Mshahara wa kuanzia ni kima cha serikali katika ngazi ya **TGS. B1**

### 2.0 MASHARTI YA JUMLA:

i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na mwenye umri usiopungua Miaka Kumi na Nane (18) na usiozidi miaka Arobaini na Tano (45).
**Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**
ii. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili
iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed CV**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (**Referees**) watatu wa kuaminika
iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma,maelezo,nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni kidato cha Nne, kidato cha Sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika. **Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificate, - vyeti vya kitaaluma (professional Certificate from respective boards)**
v. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU/NACTE na NECTA)**
vi. “Testimonials”, Provisional Results, Statement of Results, Hati za matokeo za kidato cha nne na sita (**FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA**.
vii. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na.CAC45//257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010
viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa umma hawaruhusiwi kuomba isipokua kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi

ix. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria

x. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 28 Novemba 2024.

xi. **MUHIMU** kumbuka kuambatanisha Barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya Elimu, Anuani ya Barua hiyo ielekezwe kwa;

MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI,
S.L.P 42,
SINGIDA.

xii**.** ***Maombi yote yatumwe kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia Anuani ifuatayo http://portal.ajira.go.tz, Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa "Recruitment Portal".***

xii. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioidhinishwa katika Tangazo hili Hayatafanyiwa Kazi**

xiii. limetolewa na;

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI**